# SHIRIKISHO LA MPIRA WA KIKAPU TANZANIA

# KATIBA

TOLEO LA 3

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

NOVEMBA 2020

UTANGULIZI 3

## SURA YA KWANZA: JINA, MAKAO MAKUU, MATUMIZI, TAFSIRI NA MADHUMUNI

| | | | |
|---|---|---|---|
| IBARA YA | 1 | JINA | UKURASA 3 |
| IBARA YA | 2 | MAKAO | UKURASA 3 |
| IBARA YA | 3 | MATUMIZI | UKURASA 3 |
| IBARA YA | 4 | TAFSIRI | UKURASA 3 |
| IBARA YA | 5 | MADHUMUNI | UKURASA 4 |

## SURA YA PILI: JINA, MAKAO MAKUU, MATUMIZI, TAFSIRI NA MADHUMUNI

| | | | |
|---|---|---|---|
| IBARA YA | 6 | AINA ZA UANACHAMA | UKURASA 5 |
| IBARA YA | 7 | ADA NA USAJILI | UKURASA 6 |
| IBARA YA | 8 | HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA | UKURASA 6 |
| IBARA YA | 9 | HAKI YA KUPIGA KURA | UKURASA 6 |
| IBARA YA | 10 | KUPOTEZA UANACHAMA | UKURASA 7 |
| IBARA YA | 11 | KURUDISHWA UANACHAMA | UKURASA 7 |

## SURA YA TATU: MUUNDO WA SHIRIKISHO

| | | | |
|---|---|---|---|
| IBARA YA | 12 | VYOMBO VYA SHIRIKISHO | UKURASA 7 |
| IBARA YA | 13 | MKUTANO MKUU NA MAJUKUMU YAKE | UKURASA 7 |
| IBARA YA | 14 | WAJUMBE WA MKUTANO MKUU | UKURASA 8 |
| IBARA YA | 15 | KAZI ZA MKUTANO MKUU | UKURASA 8 |
| IBARA YA | 16 | MKUTANO MKUU MAALUMU | UKURASA 8 |
| IBARA YA | 17 | AKIDI KATIKA MKUTANO MKUU/MAALUM | UKURASA 9 |
| IBARA YA | 18 | KUMBUKUMBU ZA MKUTANO | UKURASA 9 |
| IBARA YA | 19 | BODI YA SHIRIKISHO | UKURASA 9 |
| IBARA YA | 20 | WAJUMBE WA BODI YA SHIRIKISHO | UKURASA 10 |
| IBARA YA | 21 | KAZI NA WAJIBU WA BODI YA SHIRIKISHO | UKURASA 10 |
| IBARA YA | 22 | KAMATI YA UTENDAJI | UKURASA 11 |
| IBARA YA | 23 | WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI | UKURASA 11 |
| IBARA YA | 24 | KAZI NA WAJIBU WA KAMATI YA UTENDAJI | UKURASA 11 |
| IBARA YA | 25 | UWAJIBIKAJI | UKURASA 11 |
| IBARA YA | 26 | AKIDI YA MIKUTANO YA KAMATI YA UTENDAJI | UKURASA 12 |
| IBARA YA | 27 | KAMISHENI | UKURASA 12 |
| IBARA YA | 28 | WAJUMBE WA KAMISHENI | UKURASA 12 |


REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL TANZANIA

## SURA YA NNE: UONGOZI


| | | | |
|---|---|---|---|
| IBARA YA | 29 | MISINGI NA MAADILI YA UONGOZI | UKURASA 12 |


## SURA YA TANO: UCHAGUZI


| | | | |
|---|---|---|---|
| IBARA YA | 30 | MKUATNO MKUU WA UCHAGUZI | UKURASA 13 |
| IBARA YA | 31 | WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA UCHAGUZI | UKURASA 13 |
| IBARA YA | 32 | SIFA ZA WAGOMBEA UONGOZI | UKURASA 13 |
| IBARA YA | 33 | KIPINDI CHA UONGOZI | UKURASA 14 |


## SURA YA SITA: VIONGOZI WA SHIRIKISHO, KAZI NA MADARAKA


| | | | |
|---|---|---|---|
| IBARA YA | 34 | VIONGOZI WA SHIRIKISHO | UKURASA 14 |
| IBARA YA | 35 | RAISI WA SHIRIKISHO | UKURASA 15 |
| IBARA YA | 36 | MAKAMU RAISI WA SHIRIKISHO | UKURASA 15 |
| IBARA YA | 37 | KATIBU MKUU | UKURASA 15 |
| IBARA YA | 38 | KATIBU MKUU MSAIDIZI | UKURASA 16 |
| IBARA YA | 39 | MWEKA HAZINA | UKURASA 16 |
| IBARA YA | 40 | MAKAMISHNA | UKURASA 16 |
| IBARA YA | 41 | WAJUMBE KAMATI ZA KAMISHENI | UKURASA 16 |
| IBARA YA | 42 | MLEZI | UKURASA 17 |
| IBARA YA | 43 | BARAZA LA WADHAMINI | UKURASA 17 |


## SURA YA SABA: MGONGANO WA MASLAHI, MIGOGORO NA RUFAA


| | | | |
|---|---|---|---|
| IBARA YA | 44 | MGONGANO WA MASLAHI | UKURASA 17 |
| IBARA YA | 45 | MIGOGORO NA RUFAA | UKURASA 18 |


## SURA YA NANE: FEDHA ZA SHIRIKISHO


| | | | |
|---|---|---|---|
| IBARA YA | 46 | MAPATO | UKURASA 19 |
| IBARA YA | 47 | MATUMIZI | UKURASA 19 |
| IBARA YA | 48 | HESABU | UKURASA 20 |


## SURA YA TISA: HATI MILIKI, NEMBO, BENDER NA LUGHA


| | | | |
|---|---|---|---|
| IBARA YA | 49 | BENDERA | UKURASA 20 |
| IBARA YA | 50 | NEMBO | UKURASA 20 |
| IBARA YA | 51 | LUGHA | UKURASA 20 |
| IBARA YA | 52 | UAMUZI WA KUVUNJA SHIRIKISHO | UKURASA 20 |
| IBARA YA | 53 | KUPITISHA KATIBA | UKURASA 21 |

## UTANGULIZI

Katiba ya shirikisho la mpira wa kikapu Tanzania ni nyaraka iliyoandaliwa kwa ajili ya kusimamia mpira wa kikapu, yenye taratibu za msingi na kanuni inayosimamia misingi ambayo shirikisho linaongozwa na kusimamia kwenye taratibu na kanuni.

Katiba hii imeandaliwa kwa namna ambayo imezingatia na kusimamia kanuni na sheria na kanuni za Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Ita itasimamia mpira wa kikapu na si kinyume chake. Katiba hii itatumikia kama kipaumbele katika kujenga muundo wa kusimamia mpira wa kikapu nchini. Katiba hii itatumika kwa mujibu wa mahitaji ya kisheria, bila kuzingatia mazingira halisi, maslahi ya wanachama wote, maslahi ya mpira wa kikapu na nafasi ya michezo ya mpira wa kikapu nchini.

Katiba hii itatumika kama chombo cha Shirikisho la Taifa (TBF) kubaki imara, kukabiliana na changamoto zitakazojitokeza, na itatumika kuwakutanisha na kuwaunganisha wanachama katika maslahi ya mchezo.

## SURA YA 1

## JINA, MAKAO MAKUU, MATUMIZI, TAFSIRI NA MADHUMUNI

### IBARA YA 1: JINA

Jina: SHIRIKISHO LA MPIRA WA KIKAPU TANZANIA- (TANZANIA BASKETBALL FEDERATION) kwa kifupi TBF. Jina hili ni badala ya Basketball Association of Tanzania kwa kifupi **BATA.**

### IBARA YA 2: MAKAO MAKUU

Makao makuu ya Shirikisho yatakuwa katika mji wa Dar es Salaam. S.L. P 42089, DAR ES SALAAM

### IBARA YA 3: MATUMIZI:

Katiba hii itatumiwa na Wanachama na kuendesha shughuli zote zinazosimamamia mpira wa kikapu nchini Tanzania. Wanachama watakuwa na katiba zao ambazo zitaonyesha kuitambua katiba hii.

### IBARA YA 4: TAFSIRI:

Maana ya maneno katika katiba hii, isipokuwa pale ambapo yameainishwa vinginevyo yatamaanisha.

| | |
|---|---|
| **TBF:** | Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania au Tanzania Basketball Federation. |
| **SHIRIKISHO:** | Maana yake ni Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania. |
| **BMT:** | Baraza la Michezo la Taifa. |
| **MSAJILI:** | Msajili wa vyama vya Michezo nchini. |
| **MIKOA:** | Kiutawala ni wanachama wa msingi katika shirikisho. |
| **FIBA:** | Shirikisho la Mchezo wa mpira wa kikapu Ulimwenguni (Federation |Internationale de Basketball) |
| **WAZIRI:** | Maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya kushughulikia Michezo nchini. |
| **BODI:** | Chombo cha Utawala katika Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania. |
| **KAMATI:** | Sekretariati ya Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania. |
| **KAMISHENI:** | Kamati zinazoshikilia maeneo ya mbalimbali ya ufanisi katika utendaji wa shirikisho. |

OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## IBARA YA 5: MADHUMUNI

Katiba hii imejumuisha malengo yafuatayo:

4.1. Kutengeneza muundo wa kiutawala utakaowezesha utoaji wa huduma muhimu zitakazofanikisha ufikiwaji wa malengo yaliyowekwa kupitia katiba hii.

4.2. Kuhamasisha, kuendeleza, kupanga na kuutangaza mchezo wa mpira wakikapu nchi nzima ili kuweka mpangilio bora unaoaminika na kutekelezeka kwa uwazi.

4.3. Kuhakikisha mchezo wa mpira wa kikapu unathaminika katika jamii pamoja na kusimamia kanuni na maadili katika nyanja zote za mchezo.

4.4. Kusimamia maadili na mali za shirikisho katika njia sahihi kwa manufaa ya mchezo.

4.5. Kuto-fungamana na hali yoyote ya kisiasa wala kidini na ubaguzi wa rangi, jinsia au vinginevyo.

4.6. Kuwa kiunganishi cha kuhamasisha na kubadilishana habari, uzoefu na shughuli mbali mbali za wadau pamoja na changamoto zozote zinazohusiana na mpira wa kikapu.

4.7. Kutumika kama kiunganishi cha kuhamasisha kubadilishana habari, uzoefu na shughuli zozote za shirikisho ikiwa na pamoja kuwa tayari kujibu maswali yote yanayohusiana na mpira wa kikapu.

4.8. Kujipanga kwa njia ya kupata hadhi ya kisheria, kuwa na jina rasmi na ofisi iliyosajiliwa.

4.9. Kusajili nembo, bendera, muhuri wa kawaida na majina ya watu ambao watakuwa wawakilishi wa Shirikisho la Kitaifa (i.e Rais na / au Katibu Mkuu).

4.10. Kuwakilisha mchezo wa mpira wa kikapu mbele ya wanachama wake, Kamati ya Kitaifa ya Olimpiki, Baraza la Michezo la Kitaifa, Mamlaka ya Umma na Serikali, Shirikisho zingine za kitaifa na FIBA.

4.11. Kuweka na kusimamia njia zote za mawasiliano kati ya wanachama, vilabu, vyama (makocha, wachezaji, waamuzi, n.k), taasisi za serikali na zisizo za kiserikali na FIBA.

4.12. Kuanzisha sera ya kifedha na kutoa rasilimali za kutosha za kifedha ili kukuza mpira wa kikapu ndani ya bajeti ya fedha ya shirikisho.

4.13. Kuanzisha muundo imara unaojitegemea wa mashindano ya kila aina ndani ya nchi.

4.14. Kuzalisha rasilimali muhimu zitakazowezesha mipango ya timu za kitaifa, ambazo zinawakilisha nchi katika mashindano mbali mbali ya kimataifa.

4.15. Kudhibiti na kusimamia uhamisho wa kitaifa na kimataifa kwa wachezaji kwa kufuata kanuni za FIBA

4.16. Kuanzisha na kusimamia kanuni za uhamisho wa ndani kwa usahihi kwa faida ya mchezo.

4.17. Kukuza na kuendeleza mashindano, kambi, semina, mikutano, kozi, kliniki, mitihani, mipango ya maendeleo, hafla, kampeni, na shughuli zingine za uendelezaji kwa wanachama na wadau wake.

4.18. Kuhakikisha kuwa kazi ya Shirikisho ni ya umma, mara kwa mara itatoa taarifa kwa wanachama wake kuhusu shughuli zake, kupitia mawasiliano ya moja kwa moja, mikutano ya kawaida, mikutano ya waandishi wa habari, kurasa za wavuti, taarifa, taarifa za umma, maandishi ya vyombo vya habari, redio na TV.

4.19. Kutoa utaratibu wa kusuluhisha mizozo yote, kuhakikisha haki na usawa vinakuwepo wakati wote.

4.20. Kuandaa na kusimamia kanuni zote za kiufundi zinazohusiana na mpira wa kikapu.

4.21. Kuanzisha utaratibu wa uanachama (udhibitisho / usajili / leseni) na kuhakikisha kwamba kila mwanachama ni halali, ana cheti cha uanachama / leseni na kuamua aina na kiasi cha ada ya uanachama kwa washiriki wote.

4.22. Kuhakikisha kuwa shughuli zote za Shirikisho ni kwa wanachama walio hai /leseni tu.

4.23. Kukuza na kuendeleza kiwango cha ufundishaji, uamuzi na usimamizi wa mchezo.

4.24. Kuhimiza upatikanaji na utumiaji wa vifaa sahihi vya mchezo.

4.25. Kujenga msimamo, uaminifu na utaratibu unaokubalika katika mazingira ya mpira wa kikapu nchini.

Katiba hii inaendana na muhula wa kipindi cha miaka 4 (mamlaka) ambayo yanaendana na Kalenda ya Shirikisho la mpira wa kikapu duniani (FIBA) (muda wa mashindano ya dunia/uchaguzi kila baada ya miaka 4)

REGIST... OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

# SURA YA 2

# UANACHAMA

## IBARA YA 6: AINA ZA UANACHAMA

### 6.1. UANACHAMA WA MSINGI

6.1.1. Shirikisho litaundwa na Mikoa ambayo ndio wanachama wake wa msingi.

6.1.2. Mikoa itasajiliwa chini ya sheria Na. 12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake Na. 6 ya 1971 ya BMT, pamoja na kanuni za usajili Na. 442 za mwaka 1999.

6.1.3. Mikoa itaundwa na Vilabu vinavyojihusisha na mpira wa kikapu na vilivyo sajiliwa na BMT.

6.1.4. Mikoa ya Shirikisho ina hadhi sawa, kila mkoa una mamlaka kamili katika eneo lake.

6.1.5. Mikoa itaheshimu katiba ya shirikisho na kutekeleza kanuni, taratibu na maamuzi yote yatakayo tolewa na vyombo vya Shirikisho.

6.1.6. Mikoa itakuwa na dhamana ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya shirikisho.

6.1.7. Mikoa itatekeleza wajibu wake kwa kuendeleza mpira wa kikapu katika mikoa na kushirikiana na vyombo vingine vya shirikisho, ili kuboresha ukuaji na ustawi wa mchezo wa mpira wa kikapu.

### 6.2. UANACHAMA WA USHIRIKA

Kutakuwa na wanachama wa kujishirikisha. Vyama vya kitaalamu vya Mprira wa kikapu vitakuwa ni wanachama wa kujishirikisha ikiwa ni pamoja na:

6.2.1. Chama cha waalimu wa Mpira wa Kikapu Tanzania

6.2.2. Chama cha waamuzi wa mpira wa Kikapu Tanzania

6.2.3. Chama cha mpira wa Kikapu kwa watu wenye ulemavu Tanzania

6.2.4. Asasi za michezo ngazi ya Taifa zinazojihusisha na mpira wa kikapu kama ilivyo ainishwa katika katiba ya asasi hizo.

### 6.3. UANACHAMA WA HESHIMA

Kutakuwa na wanachama wa heshima wa TBF. Bodi ya Shirikisho inaweza kutoa uanachama wa heshima kwa watu mashuhuri waliotoa mchango uliotukuka kwa shirikisho, au Chama cha hiari au Taasisi yoyote kutokana na mchango wao kwenye maendeleo ya mpira wa kikapu.

## IBARA YA 7: ADA NA USAJILI

7.1. Kila anayetaka kuwa mwanachama atatuma maombi yakiambatana na kiingilio na ada ya Uanachama kabla ya kukubaliwa.

7.2. Kutakuwa na kiingilio kwa mwanachama mpya na ada ya kila mwaka.

7.3. Viwango vya ada na viingilio vitapangwa na Bodi na vinaweza kubadilishwa inapobidi kufuatia mabadiliko ya kanuni za Shirikisho.

7.4. Maombi ya uanachama yakikataliwa kwa sababu zozote; Katibu Mkuu atamjulisaha aliyekataliwa maombi yake akimtajia kasoro zilizopo. Ada zitarudishwa iwapo maombi yatakataliwa kabisa.

7.5. Kila mwanachama wa kujishirikisha, atatuma maombi kwa katibu mkuu wa TBF kwa kutumia fomu maalum itakayotolewa na SHirikisho.

7.6. Mwanachama mpya wa msingi atakubaliwa na kamati ya utendaji mara moja endapo atakidhi vigezo.

## IBARA YA 8: HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA

Mwanachama atakuwa na wajibu na haki zifuatazo:

8.1. Mwanachama atakuwa na haki ya kushiriki mikutanao ya shirikisho inayomhusu.

8.2. Kushiriki mashindano yanayoandaliwa na shirikisho yanayomhusu.

8.3. Atakuwa na haki ya kuchagua viongozi wa shirikisho katika ngazi yake.

8.4. Mwanachama atakuwa na haki ya kuomba uongozi na kuchaguliwa kwa mujibu wa katiba hii.

8.5. Kila mwanachama atawajibika kutekeleza majukumu yake kikatiba chini ya usimamizi wa Shirikisho kupitia kanuni, taratibu na sheria zote zinazosimamia mchezo wa mpira wa kikapu.

8.6. Kila mwanachama atawajibika kuwasilisha taarifa zake za uendeshaji kama ilivyo ainishwa katiba ibara ya 18 kifungu kidogo 18.2 (v).

## IBARA YA 9: HAKI YA KUPIGA KURA

Katika makundi yote ya uanachama yaliyotajwa hapo juu, wanachama wenye haki za kupiga kura watakuwa ni wale walio na uanachama wa msingi na washirika kupitia mfumo wa kupigia kura.

### 9.1. MFUMO WA KUPIGA KURA KWA WAJUMBE

Kila Mwanachama wa msingi na ushirika atakuwa na kura 1.

### 9.2. LESENI

Kila mchezaji, mwalimu, mwamuzi, msimamizi wa mchezo, mkufunzi, daktari, nk wanapaswa kuwa na leseni ya Shirikisho na wote wana haki ya kutumia leseni zao kwenye vyama vyao vya kitaaluma.

OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## IBARA YA 10 : KUPOTEZA UANACHAMA

Mwanachama kama alivyotajwa katika katiba hii,atapoteza sifa ya uanachama iwapo yatatokea mojawapo ya mambo yafuatayo:

10.1. Atashindwa kulipia ada ya uanachama katika muda wa miaka mitatu (3) mfululizo.
10.2. Atafutwa na kusimamishwa na msajili kwa mujibu wa sheria ya BMT.
10.3. Atakiuka na kuvunja kanuni na taratibu za Shirikisho.
10.4. Atakiuka na kuvunja kwa makusudi katiba ya TBF kiasi cha kuathiri maendeleo ya mpira wa kikapu nchini.

## IBARA YA 11: KURUDISHIWA UANACHAMA

Mwanachama aliyepoteza uanachama wa TBF kama ilivyo katika ibara ya 9 anaweza kurejeshewa uanachama wake iwapo:

11.1. Atalipa ada zote alizokuwa akidaiwa.
11.2. Atarejeshewa au kusajiliwa upya na msajili.
11.3. Atakiri na kuomba msamaha kwa maandishi kwenye bodi ya shirikisho kutokana na makosa yaliyofanya apoteze uanachama wake.

# SURA YA 3

# MUUNDO WA SHIRIKISHO

## IBARA YA 12: VYOMBO VYA SHIRIKISHO

Kutakuwepo na vyombo vifuatavyo katika shirikisho

1. Mkutano Mkuu
2. Bodi ya Shirikisho
3. Kamati ya utendaji
4. Kamati ya Sheria, Maadili na Nidhamu
5. Kamisheni za shirikisho
6. Baraza la Udhamini

OF SPORTS ASSOCIATION
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## IBARA YA 13: MKUTANO MKUU NA MAJUKUMU YAKE

Mkutano mkuu ndicho chombo chenye mamlaka ya juu kuliko vyombo vingine na ndicho kitakuwa na maamuzi ya mwisho katika mambo yote yanayohusu ustawi na maendeleo ya mpira wa kikapu nchini Tanzania.

13.1. Mkutano mkuu utaitishwa mara moja kila baada ya miaka 2 lakini unaweza kuitishwa kwa dharura endapo kuna haja na ulazima wa kufanya hivyo.
13.2. Mkutano mkuu utaitishwa na Rais wa Shirikisho baada ya mashauriano na Kamati ya Utendaji.
13.3. Bodi ya shirikisho inaweza kwa maombi ya maandishi ya wajumbe wasiopungua nusu ya wajumbe wa Mkutano mkuu.
13.4. Taarifa ya Mkutano mkuu sharti itolewe kwa maandishi kwa wajumbe sio chini ya mwezi mmoja (siku 30) kabla ya tarehe ya kikao.

13.5. Idadi ya wajumbe kwenye mkutano Mkuu sharti isipungue zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa mkutano Mkuu wenye haki ya kupiga kura.
13.6. Endapo idadi ya wajumbe waliohudhuria haifikii kiwango zaidi ya nusu, mkutano utahairishwa kwa muda usiopungua siku 60.
13.7. Kutakuwepo na mkutano mkuu wa uchaguzi kila baada ya miaka minne (4).
13.8. Mkutano Mkuu utachagua viongozi wa shirikisho.

## IBARA YA 14: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU

Kutakuwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kupitia nafasi zao kama ifuatavyo:

14.1. Raisi wa Shirikisho.
14.2. Makamu wa Rais wa Shirikisho.
14.3. Wajumbe wote wa kamati ya utendaji.
14.4. Mwenyekiti na katibu kutoka kila mkoa.
14.5. Mwenyekiti na katibu kutoka vyama shiriki.
14.6. Mchezaji mwakilishi kutoka katika ligi ya kila mkoa.

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## IBARA YA 15: MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU

Mkutano Mkuu pia una wajibu wa kutimiza kazi zifuatazo za Shirikisho:

15.1. Kupitisha, kurekebisha na kubadili katiba.
15.2. Kuchagua viongozi wa shirikisho.
15.3. Kuhakiki, kuchunguza na kupitisha taarifa zote (hasa taarifa za Bodi / Kamati ya Utendaji).
15.4. Kuidhinisha taarifa za akaunti na mahesabu pamoja na bajeti ya Shirikisho
15.5. Kupitisha kanuni za ndani.
15.6. Kuteua mkaguzi wa mahesabu.
15.7. Kupiga kura ya kutokuwa na imani kwa Bodi au Kamati ya Utendaji.
15.8. Kutoa mapendekezo ya Patron na Wanachama wa heshima.
15.9. Kuthibitisha / kuondoa viongozi / wanachama wa Shirikisho.
15.10. Kusimamia, kuelekeza au kuagiza cha kufanya au kutekelezwa na vyombo vilivyo chini kwa maendeleo ya mpira wa kikapu.
15.11. Kurekebisha, kubadilisha, kuthibitisha na kuidhinisha uamuzi wowote uliotolewa na vyombo vya chini kama hapana budi.
15.12. Kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kumvua madaraka kiongozi yeyote wa Taifa au ngazi ya chini, au kufuta uanachama wa mwanachama yeyote.

## IBARA YA 16: MKUTANO MKUU MAALUM

16.1. Mkutano Mkuu pia inaweza kukutana kupitia Mkutano Mkuu maalum, kukiwa na ulazima.Unaweza kuitishwa kupitia ombi la Bodi/ Kamati ya utendaji au asilimia 51% ya wanachama wenye haki za kupiga kura.
16.2. Iwapo Mkutano mkuu maalum utaitishwa, mambo yatakayo jadiliwa lazima yabainishwe kama ajenda katika ombi la kikao hiki.
16.3. Mambo ambayo huangukia ndani ya mamlaka ya Mkutano Mkuu yanawekwa kwenye ajenda.
16.4. Mkutano Mkuu maalum unapaswa kuitishwa kwa namna ile ile kama Mkutano Mkuu wa kawaida ndani ya siku 21 baada ya kupokea ombi la mkutano.

## IBARA YA 17: AKIDI KATIKA MKUTANO MKUU NA MKUTANO MKUU MAALUM

17.1. Akidi (idadi ndogo ya wanachama wa kupigia kura kuweza kupitisha maazimio) kwenye Mkutano Mkuu lazima iwe zaidi ya asilimia (50% pamoja na kura moja).

17.2. Maamuzi yanapaswa kuchukuliwa na kura nyingi za wajumbe waliopo (Kuanzia asilimia 25 ya wanachama wote pamoja na kura moja inahitajika kwa uamuzi wowote).

17.3. Kwa baadhi ya maamuzi muhimu, (kwa mfano kwa mabadiliko ya katiba, mfumo wa mashindano, uhamisho na usajili wa wachezaji, n.k.) idadi kubwa kabisa (kuanzia 50% pamoja na kura moja ya wanachama wote ) inahitajika kupitisha maamuzi.

17.4. Wakati wa Mkutano Mkuu Maalum unafanyika, utaratibu wa akidi utaendelea kutumika kama ilivyo kwenye Mkutano Mkuu.

## IBARA YA 18: KUMBUKUMBU ZA MKUTANO

Katiba inasisitiza kwamba shirikisho litaendeshwa katika msingi ya kidemokrasia. Msingi ambao utahusisha mikutano, ambapo mazungumzo hufanyika na maamuzi yanafanywa.

18.1. Wanachama watataarifiwa juu ya mkutano kwa njia ya "Taarifa ya Mkutano" na taarifa hii pia itaonyesha vitu vitakavyojadiliwa katika mkutano huo yaani kama Ajenda.

18.2. Vitu na utaratibu ambao utazingatiwa kama sehemu ya ajenda ni:

i. **Mahudhurio na kuanzisha kikao**

ii. **Kupitia kumbukumbu za mkutano uliopita**
Kumbukumbu za mkutano uliopita lazima zithibitishwe na kusahihishwa. Marekebisho yoyote lazima yakubaliwe, Marekebisho yote lazima yaingizwe kwenye kumbukumbu za mkutano wa sasa.

iii. **Kumbukumbu za yatokanayo na mkutano uliopita**
Taarifa yoyote inayotokana na kumbukumbu za mkutano uliopita yanaweza kutolewa wakati huu kama sehemu ya mwendelezo wa kikao husika. Hatua zozote zilizochukuliwa kutokana na maamuzi yaliyofanywa katika mkutano uliopita zinapaswa kutolewa taarifa.

iv. **Taarifa ya Fedha**
Kupokea taarifa kutoka kwa Mweka Hazina.

v. **Taarifa ya Utendaji**
Kupokea taarifa ya utendaji wa shirikisho kutoka kwa Katibu, pamoja na idhini ya ripoti za kikamisheni na shughuli za maendeleo ya mchezo katika mikoa.

vi. **Mikakati na Mpango kazi wa kipindi kijacho**
Kupokea mikakati na mpango kazi wa shughuli za shirikisho kwa kipindi kijacho kulingana na majukumu na malengo ya shirikisho.

vii. **Mengineyo**
Hii ni wakati hoja na mijadala mingine ambayo haijaorodheshwa kwenye ajenda inaweza kujadiliwa, **kawaida ni kwa idhini ya Mwenyekiti**.

viii. **Tarehe ya Kikao Kinachofuata**
Ikiwa Shirikisho halina tarehe za mapema za mikutano yake ni muhimu kuuliza washiriki wakati gani itakuwa rahisi kufanya mkutano unaofuata ili kuepuka usumbufu na mahudhurio duni.

ix. **Kufunga Kikao**

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## IBARA YA 19: BODI YA SHIRIKISHO

19.1. Bodi ya shirikisho ndiyo chombo cha juu cha utawala cha Shirikisho kitakacho wajibika kwenye Mkutano mkuu.

19.2. Bodi ya shirikisho itaitishwa mara mbili kila mwaka.
19.3. Kunaweza kuitishwa kikao cha dharura endapo kutakuwa na haja na ulazima wa kufanya hivyo.
19.4. Kikao cha Bodi kitaitishwa na Raisi wa Shirikisho baada ya kushauriana na kamati ya Utendaji.
19.5. Wajumbe wasiopungua nusu ya wajumbe wenye haki ya kupiga kura wanaweza kuomba kimaandishi kuitishwa kwa kikao.
19.6. Taarifa ya kikao cha Bodi sharti itolewe kwa maandishi sio chini ya siku 30 kabla ya tarehe ya kikao.
19.7. Endapo idadi ya wajumbe waliohudhuria haifikii nusu ya kiwango cha wajumbe wote mkutano utahairishwa kwa muda usiopungua siku 30.

## IBARA YA 20: WAJUMBE WA BODI YA SHIRIKISHO

Wajumbe wa Bodi ya shirikisho watakuwa: -

20.1. Raisi wa shirikisho
20.2. Makamu wa Rais
20.3. Wajumbe wa kamati ya utendaji
20.4. Wenyeviti wa vyama vya mikoa na vyama shiriki bila ya kuwakilishwa.

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## IBARA YA 21: KAZI NA WAJIBU WA BODI YA SHIRIKISHO

Bodi ya Shirikisho itakuwa na kazi na majukumu yafuatayo:

21.1. Bodi kitakuwa ndicho chombo chenye mamlaka ya juu, ambacho kitatekeleza kusimamia na kupanga utekelezaji wa shughuli za mpira wa kikapu nchini Tanzania.
21.2. Kufanya matayarisho ya mkutano mkuu.
21.3. Kupokea na kujadili taarifa za kamati ya utendaji na kuchukua hatua ipasavyo.
21.4. Kupokea na kujadili taarifa za mikoa.
21.5. Kutayarisha kutoa taarifa za shirikisho.
21.6. Kuwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya shirikisho mbele ya mkutano mkuu.
21.7. Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya mkutano mkuu.
21.8. Kujadili na kupitisha bajeti ya shirikisho.
21.9. Kupokea, kupanga na kuthibitisha kanuni za shirikisho.
21.10. Kupokea na kuthibitisha sheria za michezo.
21.11. Kupendekeza majina matatu ya watu mashuhuri kwenye mkutano mkuu, watakao unda Baraza la wadhamini.
21.12. Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya kiongozi au uongozi wa chama au klabu, mwamuzi, na mchezaji kutokana na kukiuka kanuni za shirikisho au kanuni za uendeshaji Ligi au mashindano yeyote ya mpira wa kikapu.
21.13. Kuteua au kujaza nafasi za uongozi zitakazo kuwa wazi, isipokuwa ile ya Rais wa Shirikisho na Makamu wake.
21.14. Kuwateua Makamishna kwa misingi ya sifa kwa kamisheni zote [zilizotajwa katika kifungu 4.5] kwa misingi ya mikataba yenye uwezekano wa kuongezwa kipindi cha miaka miwili miwili.
21.15. Kila kamisheni itapewa hadidu za rejea (Terms of Reference) ambazo zita akisi (reflect) madhumuni na malengo ya shirikisho kwenye kamisheni husika.
21.16. Majina yaliyoteuliwa yatawasilishwa kwenye mkutano mkuu utakaofuata kwa kuthibitishwa.
21.17. Kusitisha uanachama wa mwanachama yeyote atakaye kiuka Katiba hadi suala hilo litakapo amuliwa vinginevyo na mkutano mkuu.
21.18. Kufanya kazi yoyote ile kwa manufaa na ustawi wa mpira wa kikapu nchini.
21.19. Kupendekeza hatua stahiki za kinidhamu dhidi ya mwanachama yeyote.

## IBARA YA 22: KAMATI YA UTENDAJI

Inasimamia shughuli zote za kiutendaji za shirikisho, ikiwa ni pamoja na kutekeleza maamuzi yote yaliyotolewa kwenye Mkutano Mkuu / Mkutano wa Bodi.

Kamati ya utendaji kitakuwa ni chombo cha watendaji wa kazi za kila siku za shirikisho. Kamati ya utendaji kwa maana ya ufanisi wa shirikisho, itakuwa ndiyo Sekretarieti ya TBF.

## IBARA YA 23: WAJUMBE WA KAMATI YA UTENDAJI

Kamati ya Usimamizi itaunda maafisa wafuatao watakaohusika na utekelezaji wa shughuli za kila siku za Shirikisho:

1. Rais
2. Katibu Mkuu
3. Mweka Hazina
4. Makamishina wa Shirikisho

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

Rais atakuwa mwenyekiti wa kamati ya utendaji na Katibu Mkuu atakuwa katibu wake.

## IBARA YA 24: KAZI NA MAJUKUMU YA KAMATI YA UTENDAJI

24.1. Kamati ya Utendaji lazima ifanye shughuli zake / miradi yake kwa faida ya mpira wa kikapu. Majukumu yote ya Kamati ya Utendaji ni lazima yashabihiane na malengo ya Shirikisho.
24.2. Kusimamia na kutoa mwelekeo katika maswala ya mpira wa kikapu, kwa faida ya mchezo.
24.3. Kusimamia na kutekeleza sera, maamuzi na mapendekezo mbali mbali toka katika vikao vya Bodi na Mkutano Mkuu
24.4. Kubuni na kupanga mbinu za utekelezaji wa maagizo ya Bodi ya shirikisho kwa ufanisi.
24.5. Kusimamia sera za kimataifa za Shirikisho kwa maendeleo ya mchezo.
24.6. Kupokea na kufanyia kazi maombi ya uanachama.
24.7. Kuteua makocha na wasimamizi wa timu ya Taifa.
24.8. Kuteua wawakilishi wa Shirikisho katika vyombo mbali mbali vya kiserikali na visivyo vya serikali vya michezo.
24.9. Kuandaa Kalenda ya shughuli za Shirikisho.
24.10. Kutayarisha ajenda za kikao cha Bodi.
24.11. Kudhibiti usimamizi wa jumla wa kifedha wa Shirikisho na kutoa ripoti kwa Bodi na Mkutano Mkuu.
24.12. Kupokea na kujadili taaarifa za kamisheni.
24.13. Kupokea na kufanya maamuzi ya rufani.
24.14. Kupitisha na kurekebisha sheria, kanuni za ndani na miongozo.
24.15. Kukabidhi baadhi ya majukumu kwa kamati au vyama.
24.16. Kupitia na kuthibitisha kanuni na miongozo ya kamati na vyama vya mikoa.
24.17. Kutekeleza shughuli zote ambazo ziko nje ya mamlaka ya Mkutano Mkuu.
24.18. Kukusanya na kuthibitisha taarifa zote kuhusu wachezaji, walimu, waamuzi na wadau wengine wa Mpira wa Kikapu.
24.19. Kupendekeza jina la mlezi
24.20. Kuhakikisha kuwa katiba, kanuni na taratibu za kuongoza mpira wa kikapu nchini zinafuatwa na kuzingatiwa.

## IBARA YA 25: UWAJIBIKAJI

Wajumbe wa Kamati ya utendaji (i.e. mmoja mmoja au kwa pamoja) watawajibika kwa Bodi na Mkutano Mkuu.

## IBARA YA 26: AKIDI YA MIKUTANO YA KAMATI YA UTENDAJI

Akidi katika mikutano ya Kamati ya Utendaji inapaswa kuwa (50% pamoja na mtu mmoja) na maamuzi yanapaswa kuchukuliwa kwa utaratibu huo (i.e. kura za wanachama wa Kamati ya Utendaji).

Ikitokea kura zimelingana, Mwenyekiti ana kura ya maoni. Inapendekezwa kuwa Kamati ya Utendaji inapaswa kukutana angalau mara moja kwa mwezi.

## IBARA YA 27: KAMISHENI

27.1. Shirikisho litakuwa na kamisheni kumi (10) ambazo ni :-
- 27.1.1. Kamisheni ya Makocha.
- 27.1.2. Kamisheni ya Waamuzi.
- 27.1.3. Kamisheni ya watoto na maendeleo ya vijana.
- 27.1.4. Kamisheni ya Wanawake.
- 27.1.5. Kamisheni ya Mipango na Maendeleo.
- 27.1.6. Kamisheni ya watu wenye ulemavu.
- 27.1.7. Kamisheni ya Tiba ya wanamichezo.
- 27.1.8. Kamisheni ya ufundi na uendeshaji wa mashindano.
- 27.1.9. Kamisheni ya Habari, mawasiliano na masoko.
- 27.1.10. Kamisheni ya Kikapu cha 3x3 na Michezo ya Mtandaoni (E-Sports)

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

27.2. Kila kamisheni itaongozwa na Kamishna ambaye atakuwa ameteuliwa na bodi ya shirikisho.

27.3. Kamishina atakuwa mwenye dhamana ya kuteua wajumbe watakao msaidia kuongoza kamisheni.

27.4. Kamisheni itakutana mara moja kila mwezi ila inaweza kuitisha mkutano wa dharura wa kamisheni iwapo kuna ulazima wa kufanya hivyo.

## IBARA YA 28: WAJUMBE WA KAMISHENI

28.1. Kamishina ataunda kamisheni kwa muundo unaofaa.

28.2. Mwenyekiti wa vikao vyote vya kamisheni atakuwa ni kamishina mwenyewe.

28.3. Kutakuwepo na wajumbe wa kamisheni wasiozidi watano na wasiopungua watatu.

28.4. Wajumbe hao watateuliwa na kamishina anayehusika na kuthibitishwa na kamati ya utendaji.

28.5. Wajumbe watawajibika kwa kamishina mhusika na kwenye kamati ya utendaji.

# SURA YA 4

# UONGOZI

## IBARA YA 29: MISINGI NA MAADILI YA UONGOZI

29.1. Ni kwa manufaa ya Shirikisho kwamba wajumbe wote wa Bodi na Kamati ya Utendaji ni wenye uadilifu wa hali ya juu na wana uelewa juu ya utawala bora.

29.2. Ikiwa mjumbe wa Bodi au Kamati ya Utendaji atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo ya Bodi au Kamati bila maelezo ya kujitosheleza, anapaswa kupewa onyo toka Bodi /Kamati ya Utendaji.

29.3. Kama jambo (29.2) likijitokeza, Rais atakuwa na haki ya kuteua mjumbe mpya wa Kamati ya Utendaji hadi Mkutano wa Bodi ujao utakapothibitisha.

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATIONS & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

# SURA YA 5

# UCHAGUZI

## IBARA YA 30: MKUATNO MKUU WA UCHAGUZI

30.1. Kutakuwepo na mkutano mkuu wa uchaguzi kila baada ya miaka minne (4).

30.2. Mkutano mkuu unaweza kuridhia na kuongeza muda wa kuendelea na uongozi uliopo au unaweza kuteua kamati ya muda ya uongozi na kuipa kipindi maalumu cha kuongoza na kuitisha mkutano wa uchaguzi.

30.3. Siku 30 zikipita baada ya kipindi cha uongozi kumalizika bila ridhaa ya mkutano mkuu, viongozi wanaomaliza muda wao watahesabika kuwa wamejivua uongozi.

30.4. Uchaguzi wa T.B.F utakuwa ni wa haki na uwazi na utasimamiwa na BMT.

30.5. Katika hatua hii Baraza la Michezo (B.M.T) litaandaa utaratibu wa kuitisha uchaguzi ili kuchagua uongozi mpya.

30.6. Mkutano mkuu ukitoa ridhaa yake, kwa uongozi uliopo madarakani kama unavyoelezeka katika (kifungu 30.2 hapo juu) ridhaa hiyo itakuwa kwa kipindi kisichozidi siku 90 (tisini tu) baada ya siku ya mwisho ya kipindi cha uongozi kumalizika.

30.7. Fomu za wagombea zitatolewa na B.M.T. Aidha BMT itafanya uchambuzi wa majina ya wagombea kwa kuzingatia sifa za wagombea kama zilivyoainishwa katika katiba ya T.B.F.

30.8. Mkutano mkuu wa uchaguzi utachagua na kujaza nafasi zifuatazo:

- 30.8.1. Rais wa Shirikisho.
- 30.8.2. Makamu wa Rais.
- 30.8.3. Katibu Mkuu.
- 30.8.4. Katibu Mkuu Msaidizi

Shughuli za uchaguzi zitaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi za T.B.F na zile za FIBA.

## IBARA YA 31: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA UCHAGUZI

31.1. Wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi ni wale tu ambao wameainishwa kwenye ibara ya 14 na wawe hawadaiwi ada ya mwaka.

31.2. Mwenyekiti na katibu kutoka kila mkoa mwanachama watakuwa wajumbe wenye haki ya kupiga kura.

31.3. Mwenyekiti na makatibu kutoka vyama vishiriki watakuwa wajumbe wenye haki ya kura moja.

31.4. Mchezaji mwakilishi kutoka kila mkoa mwanachama uliofanya ligi atakuwa na haki ya kupiga kura.

31.5. Wajumbe wa kamati ya utendaji wanaomaliza muda wao hawatapiga kura wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi.

31.6. Msimamizi wa uchaguzi mkuu kutoka BMT ambaye hatapiga kura.

## IBARA YA 32: SIFA ZA WAGOMBEA UONGOZI

Wagombea wa uongozi wa Shirikisho wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo:

32.1. Awe na umri usiopungua miaka 25, isipokuwa wale wanaogombea nafasi ya Rais na Makamu wa Rais ambao wanatakiwa wawe na umri usiopungua miaka 30.

32.2. Awe raia wa Tanzania.

32.3. Awe na elimu angalau ya kidato cha nne.

32.4. Awe na ufahamu juu ya Shirikisho na Taasisi zake, ajue shughuli zake na uendeshaji.

32.5. Awe na uzoefu juu ya nafasi ya uongozi anayogombea.

32.6. Awe na uwezo wa kuzungumza na kuandika lugha ya kiswahilil na kiingereza ambazo zinatumiwa na Shirikisho.

32.7. Awe na moyo wa kujitolea na awe na nafasi ya kutoa muda wake kwa kutumikia Shirikisho bila ya malipo kwa kipindi tofauti angalau siku 90 kwa mwaka. Akishiriki katika vikao, warsha na mashindano.
32.8. Awe hajapatikana na hatia ya kosa lolote la jinai hususa linalogusa na kushusha hadhi, utu na haiba mbele ya jamii (kama ubadhirifu, wizi, mauaji, kubaka, madawa ya kulevya n.k.)
32.9. Awe na akili timamu na hajawahi kuugua ugonjwa wa akili.
32.10. Wagombea wa nafasi ya Rais na Makamu wake, lazima wawe na elimu na uzoefu wa kutosha wa mambo ya utawala wa michezo, hasa wawe wameisha wahi kuongoza mchezo wa mpira wa kikapu kwa ngazi yoyote nchini.
32.11. Awe amewahi kuwa mchezaji wa mpira wa kikapu, au kuhudhuria mafunzo ya ualimu wa mpira wa kikapu, uamuzi, utawala wa michezo, tiba ya wanamichezo, au utunzaji na utengenezaji wa viwanja vya michezo.

## IBARA YA 33: KIPINDI CHA UONGOZI

Kipindi cha uongozi wa shirikisho ni miaka mine.

33.1. Kiongozi yoyote wa TBF anaweza kuchaguliwa kuongoza kwa vipindi visivyozidi viwili (2) vya uongozi katika nafasi moja.
33.2. Kiongozi ambae atajiuzulu uongozi katika nafasi fulani baada ya kuitumikia kwa zaidi ya miaka mitatu atahesabika kuwa ametumikia kipindi kizima.
33.3. Endapo kutatokea nafasi ya wazi ya uongozi kutokana na sababu yoyote, nafasi hiyo itajazwa na mamlaka zenye dhamana hiyo kwa mujibu wa katiba hii katika kikao kinachofuata.

# SURA YA 6

# VIONGOZI WA SHIRIKISHO, KAZI NA MADARAKA

## IBARA YA 34: VIONGOZI WA SHIRIKISHO

Kutakuwa na viongozi wa shirikisho wafuatao:

34.1. Rais wa Shirikisho
34.2. Makamu wa Rais
34.3. Katibu Mkuu
34.4. Katibu Mkuu msaidizi
34.5. Mweka Hazina
34.6. Makamishina wa kusimamia utendaji wa kamisheni zifuatazo:
  i. Mipango na maendeleo
  ii. Watoto na maendeleo ya vijana
  iii. Wanawake
  iv. watu wenye ulemavu
  v. Makocha
  vi. Waamuzi
  vii. Tiba ya wanamichezo.
  viii. Ufundi na uendeshaji mashindano
  ix. Habari, mawasiliano na masoko
  x. Kikapu cha 3x3 na Michezo ya mtandaoni (i.e. E-Sports)

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
SPORTS COUNCIL

## IBARA YA 35: RAISI WA SHIRIKISHO

Mkutano Mkuu unachagua Rais anayestahili kusimamia Mkutano Mkuu, lakini wakati huo huo ana jukumu la kuendesha Mkutano.

35.1. Rais pia atakuwa mjumbe wa Bodi ya shirikisho na atasimamia mikutano yake (i.e. Mwenyekiti).
35.2. Rais atawakilisha Shirikisho mbele ya umma.
35.3. Ikitokea kura zimefungana katika mikutano, Rais atakuwa na kura ya maoni.
35.4. Atakuwa kiongozi mkuu wa shirikisho mwenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa madhumuni ya shirikisho.
35.5. Atapitisha malipo kwa kutia saini kwenye hundi za shirikisho.
35.6. Ataweka saini mikataba yote inayohusu Shirikisho.
35.7. Atahakikisha kuwa shughuli zote za kila siku za Shirikisho zinaendeshwa kwa mujibu wa taratibu za ufanisi na madhumuni ya shirikisho.
35.8. Atafuatilia kuona kuwa maagizo yote yatokayo kwenye vyombo vya juu kwa Shirikisho yanatekelezwa ipasavyo na Kamati ya Utendaji.
35.9. Atawajibika kulinda na kuitetea kwa nguvu zake zote katiba ya Shirikisho kwa manufaa ya mchezo.
35.10. Atakuwa Mdhibiti Mkuu wa shughuli na maendeleo ya watumishi wote walioajiriwa na Shirikisho. (i.e. Manages)
35.11. Anaweza kufanya maamuzi yoyote ya dharura kwa kuishirikisha Bodi ya shirikisho kama jambo linalofanyiwa maamuzi lipo nje ya kanuni na taratibu za Shirikisho.
35.12. Anaweza kushiriki katika kikao chochote cha shirikisho kwenye ngazi ya chini.
35.13. Atawajibika kwenye bodi ya shirikisho na Mkutano Mkuu.

## IBARA YA 36: MAKAMU RAISI WA SHIRIKISHO

36.1. Atakuwa na kazi na madaraka yote ya Rais kama yalivyoainishwa katika ibara ya 35, iwapo Rais wa Shirikisho hayupo.
36.2. Atajishughulisha na ustawi wa matawi ya shirikisho na kuhamasisha kujiunga kwa wanachama wapya.
36.3. Atamwakilisha Rais na kufanya kazi atakazoelekezwa naye.
36.4. Atawajibika kwenye bodi ya shirikisho.
36.5. Atasimamia uwajibikaji na utekelezaji wa malengo ya shirikisho kwa wanachama wa msingi wa shirikisho.

## IBARA YA 37: KATIBU MKUU

37.1. Atakuwa afisa Mtendaji Mkuu wa Shirikisho mwenye dhamana ya kusimammia utekelezaji wa madhumuni na malengo ya shirikisho.
37.2. Atakuwa mhamasishaji mkuu wa shughuli za shirikisho na mwenezi wa mpira w kikapu.
37.3. Atakuwa ndie afisa mhasibu mkuu wa shirikisho.
37.4. Atakuwa katibu wa mkutano mkuu Bodi ya shirikisho.
37.5. Atasimamia utayarishaji wa makisio ya mapato/matumizi ya mwaka pamoja na taarifa ya fedha ya chama kwa mwaka.
37.6. Atakuwa msimamizi wa shughuli za maendeleo ya watumishi walioajiriwa na TBF. (i.e Supervise)
37.7. Anaweza kushiriki katika kikao cha kamisheni yoyote au kamati nyingine yeyote itakayoundwa.
37.8. Atatekeleza majukumu yoyote yatakayo ainishwa kwenye hadidu zake za rejea zitakazo kuwa zinapitiwa mara kwa mara katika kipindi chake cha utendaji.
37.9. Atawajibika kwa Raisi/Makamu wake na Bodi ya shirikisho.

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## IBARA YA 38: KATIBU MKUU MSAIDIZI

38.1. Atafanya kazi zote za katibu mkuu iwapo hayupo.
38.2. Atakuwa mwenyekiti wa vikao vya kuendesha mashindano mbalimbali ya shirikisho.
38.3. Atakuwa ni afisa utawala na utumishi wa shirikisho.
38.4. Atafanya kazi nyingine atakazoagizwa n kupangiwa na Katibu Mkuu au Sekretarieti/Kamati ya Utendaji.
38.5. Atakuwa katibu wa kamati ya utendaji.
38.6. Atakuwa Mwenyekiti wa Sekreatarieti, ikitokea kwamba Katibu Mkuu ambae ni mwenyekiti wa kamati hii hawezi kufika kwenye kikao hicho.
38.7. Atatekeleza majukumu yoyote yatakayo ainishwa kwenye hadidu zake za rejea zitakazo kuwa zinapitiwa mara kwa mara katika kipindi chake cha utendaji.
38.8. Atawajibika kwa Katibu Mkuu na kamati ya Utendaji.

## IBARA YA 39: MWEKA HAZINA

39.1. Atakuwa mdhibiti na msimamizi wa fedha na matumizi ya Shirikisho.
39.2. Atasimamia akaunti za shirikisho ikiwa ni pamoja na kudhibiti mapato na matumizi kwa mujibu wa bajeti.
39.3. Kuhakiki ripoti za kifedha zilizotayarishwa na sekretarieti ya Shirikisho mara kwa mara.
39.4. Kuandaa bajeti ya miaka 4 ya shirikisho kwa kushirikiana na secretariat ambayo itakuwa inapitiwa kila mwaka kwa maboresho.
39.5. Kuhakikisha matumizi sahihi ya rasilimali za shirikisho kuendana na bajeti.
39.6. Kutoa ripoti Kamili ya taarifa za fedha kwenye Mkutano Mkuu.
39.7. Atakuwa Mshauri Mkuu wa TBF kwa masula yahusuyo fedha na usimamizi wake.
39.8. Atatunza fedha na vitabu vya hesabu na nayaraka zote zihusuzo fedha.
39.9. Atakuwa mmojawapo wa kutia saini hundi za Shirikisho
39.10. Ataandaa makisio ya mapata ya shirikisho na matumizi ya fedha kwa mwaka na kuwasilisha kwenye kamati ya Utendaji.
39.11. Atatayarisha taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za shirikisho kwa mwezi, miezi mitatu na ya mwaka na kuwasilisha kwa katibu ili ijadiliwe na kamati tayari kwa ukaguzi wa mahesabu.
39.12. Atabuni njia mbalimbali za kuongeza mapato ya Shirikisho.
39.13. Atatekeleza majukumu yoyote yatakayo ainishwa kwenye hadidu zake za rejea zitakazo kuwa zinapitiwa mara kwa mara katika kipindi chake cha utendaji.
39.14. Atawajibika kwa Kamati ya Utendaji na Bodi ya Shirikisho.

## IBARA YA 40: MAKAMISHNA

40.1. Watakuwa Wenyeviti wa vikao vyote vinavyohusu kamisheni zao.
40.2. Watakuwa viongozi wenye dhamana ya kusimamia na kutekeleza shughuli zote zilizo chini ya kamisheni zao.
40.3. Watahusika na utawala wa siku kwa siku wa Kamisheni wanazoziongoza
40.4. Watateua wajumbe wa kamisheni wanazoongoza.
40.5. Watawakilisha shirikisho kwenye kongamano zinazo husiana na kamisheni zao.
40.6. Watatekeleza majukumu yoyote yatakayo ainishwa kwenye hadidu zao za rejea zitakazo kuwa zinapitiwa mara kwa mara katika kipindi cha utendaji kulingana na dira na madhumuni ya shirikisho.
40.7. Watawajibika mmoja mmoja au jumla kwenye Kamati ya Utendaji na Bodi ya Shirikisho.

## IBARA YA 41: WAJUMBE WA KAMATI ZA KAMISHENI

41.1. Watasimamia vituo vya mashindano.
41.2. Watakuwa watekelezaji wa maamuzi ya kamisheni zao

41.3. Watakuwa ni nguzo muhimu za shirikisho katika utendaji wa siku kwa siku.
41.4. Watawakilisha makamishina kwenye makongamano na warsha mbalimbali ndani na nje ya nchi.
41.5. Watachagua katibu wa Kamisheni kutoka miongoni mwao.
41.6. Watawajibika kwenye kamisheni zao na kwa kamishina mhusika.

## IBARA YA 42: MLEZI

Kutakuwepo na Mlezi atakayeteuliwa na Bodi kuthibitishwa katika mkutano mkuu.

42.1. Mlezi atakuwa mshauri mkuu wa mambo yote ya maendeleo ya mpira wa kikapu na pia atakuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini.
42.2. Mlezi atashika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mine lakini anaweza kuchaguliwa tena.
42.3. Mlezi atakuwa Mshauri wa Shirikisho na atalinda na kuitetea katiba ya shirikisho.
42.4. Mlezi anaweza kuhudhuria kikao chochote cha shirikisho katika ngazi yoyote.

## IBARA YA 43: BARAZA LA WADHAMINI

Kutakuwepo na baraza la wadhamini litakaloteuliwa na bodi na kuthibitishwa na mkutano mkuu.

43.1. Baraza la wadhamini litaundwa na wajumbe watatu, (i.e. Mlezi, na wajumbe wengine wawili (2)) watakao teuliwa na Bodi ya shirikisho.
43.2. Wajumbe wa Baraza la Wadhamini watateuliwa na kuthibitishwa na Bodi.
43.3. Wajumbe wa baraza la Wadhamini watashikiria nafasi hizo kwa kipindi cha miaka minne lakini wanaweza kuteuliwa tena.
43.4. Mali yote ya shirikisho inayoondosheka na isiyoondosheka itakuwa chini ya miliki ya baraza la wadhamini.

# SURA YA 7

# MGONGANO WA MASLAHI, MIGOGORO NA RUFAA

## IBARA YA 44: MGONGANO WA MASLAHI

Katika nyakati tofauti kunaweza kutokea utata katika mchezo au shughuli za mchezo, kama ilivyo katika fani na shughuli zingine maishani na kusababisha mgongano wa maslahi. Shirikisho litakuwa na sera juu ya suala hili, kudhibiti mwenendo wa wafanyikazi, maafisa na wanachama wa Shirikisho.

Migogoro ya masilahi, ikiwa itatokea, inaweza kuharibu vibaya sifa na taswira ya Shirikisho. Wanachama, Maafisa na wafanyakazi wa Shirikisho hawataruhusiwa kuwa na ushawishi wowote ambao unaweza kupingana na maslahi bora ya mchezo au kuchafua sifa ya Shirikisho.

Kutahitajika uthibitisho wa kimaandishi kwa kila mtu (i.e. Wanachama, Maafisa na wafanyakazi wa Shirikisho) kama anatoa/anapokea huduma kwa riba ya kifedha kupitia jina la Shirikisho. Wanachama, Maafisa na wafanyakazi wa Shirikisho hawataruhusiwa bila ruhusa/kibali kufanya hivyo.

Kutakuwepo na fomu maalum kwa viongozi watakao chaguliwa zitakazo onyesha kutojihusisha na migongano ya kimaslahi.

Wajumbe, Maafisa na wafanyikazi ambao: -

SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

44.1. Wanashiriki katika biashara zozote, shughuli, manufaa ya kifedha au ya kibinafsi ambayo:
   a. Yanakinzana au kuwa na muingiliano wa kimajukumu na shughuli zao.
   b. Yanakinzana na madhumuni ya shirikisho.

44.2. Inawaweka wao au ndugu zao katika nafasi yoyote kufaidika au kupata upendeleo wowote kupitia uwepo wao kwenye Shirikisho bila kuzingatia vigezo.

44.3. Kujiweka katika nafasi ambayo wanaweza kupata faida yoyote moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja kutokana na mikataba au huduma zozote ambazo mhusika anaweza kushawishi maamuzi.

44.4. Kujinufaisha kwa njia yoyote kutokana na utumiaji wa habari na taarifa za ndani ya shirikisho.

44.5. Kutumia mali, vifaa, bidhaa, huduma au nyenzo zozote za Shirikisho kwa shughuli binafsi ambazo hazijahusishwa na utekelezaji wa majukumu rasmi.

44.6. Kukubali zawadi, ukarimu au burudani ambayo zinaweza kudhaniwa kuwa ni za upendeleo au kama takrima.

Wakati wowote Mwanachama, Afisa na mfanyakazi atakapohusika kuwa anaweza kuhusika katika mgongano wa maslahi kama ilivyoelezwa katika ibara ya 44 hapo juu, Yeye atamwambia msimamizi wake au kupitia kikao rasmi, na atatii ushauri utakaotolewa.

Ukiukaji wa vipengele 44.1 -44.6 za Katiba hii ni kujiingiza katika mgongano wa maslahi na unaweza kuzingatiwa kama sababu ya hatua za kinidhamu, pamoja na kufukuzwa kazi/kufutwa uanachama au kuvuliwa uongozi.

## IBARA YA 45: MIGOGORO NA RUFAA

45.1. Hairusiwa kwa mtu, chombo, klabu au shirikisho kufikisha suala la mgogoro wowote dhidi ya TBF katika mahakama, isipokuwa kwa masuala ya ubadhilifu au wizi wa fedha au mali za Shirikisho.

45.2. Migogoro yoyote itatatuliwa kwa kufuata masharti na taratibu zilizomo katika katika katiba hii na kufuata sheria na kanuni za BMT.

45.3. Mtu, klabu, mkoa au chombo chochote kinacho jishirikisha na TBF kitakacho kiuka masharti ya aya ya kwanza ya ibara hii, kitachukuliwa mojawapo ya hatua zifuatazo.
   a. Kusimamishwa uanachama
   b. Kusimamishwa au kusitisha ushiriki wake katika mashindano husika au.
   c. Kupigwa marufuku kuandaa na kuendesha mchezo wa mpira wa kikapu.

45.4. Mtu au chombo chochote, ikiwa ni pamoja na mchezaji, mwamuzi, mwalimu, kiongozi yeyote wa mpira wa kikapu ndani ya nchi, anayo haki ya kukata rufaa kwa chombo cha ngazi ya juu kuliko kile kilichotoa uamuzi, kupinga maamuzi yaliyotolewa dhidi yake.

45.5. Rufaa zote za mpira wa kikapu, zitafuata utaratibu kama ilivyo ainishwa kwenye kanuni za Shirikisho.

OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

# SURA YA 8

# FEDHA ZA SHIRIKISHO

## IBARA YA 46: MAPATO

46.1. Fedha zote zitakazopatikana kutokana na shughuli za mpira wa kikapu kwenye kamisheni au kamati yoyote ndogo ya TBF, zitakuwa ni mali ya shirikisho na zitatumika kwa kusudio lake lililofanywa kukusanywa kwake.

46.2. Bodi inaweza kutoa idhini ya kuhamisha akaunti au fedha za shirikisho na kuziweka kwenye udhibiti wa taasisi nyingine, mkoa kamisheni au kamati ndogo.

46.3. Mapato ya TBF yatatokana na:

a. Viingilio kutokana na wanachama wapya.
b. Ada za wanachama kila mwaka.
c. Ada inayo lipwa na waandaji wa mashindano ambao si wanachama.
d. Ada ya leseni za waamuzi wa kitaifa.
e. Viingilio katika mashindano kutoka kwenye timu na viingilio vya uwanjani.
f. Ruzuku kutoka serikalini, TOC au mashirikisho ya kimataifa ya mpira wa kikapu.
g. Mapato yatokanayo na kutolewa kwa leseni ya kutumia haki ya shirikisho kwenye matangazo ya biashara.
h. Udhamini kupitia shughuli mbali mbali za mchezo.
i. Faini zitokanazo na adhabu kwa makosa mbalimbali.
j. Michango ya hiari.
k. Shughuli zitakazoendeshwa na TBF kuchangia shughuli maalumu za mpira wa kikapu.
l. Wakala wa matangazo anaweza kutumika kutafuta udhamini wa matangazo au kuwakilisha shirikisho kwenye majadiliano yahusuyo kifungu XX na kulipwa asilimia ya mapato kadri ya mapatano.
m. Wakala au washauri watakaowezesha mkataba wa udhamini wa shughuli za shirikisho, watalipwa asilimia itakayo kubalika, ambayo itakuwa imeongezwa kwenye mkataba wakati wa majadiliano.
n. Haki za udhamini na vipengele vya mikataba vitalindwa na kuheshimiwa.

## IBARA YA 47: MATUMIZI

47.1. Fedha za shirikisho zitatunzwa katika Akaunti ya TBF.

47.2. Malipo yote yatafanywa kufuata kanuni za fedha na kumbukumbu zote kutunzwa katika vitabu vya hesabu vya shirikisho.

47.3. Fedha zitatolewa kutoka Benki baada ya kuandikwa kwa hundi ambayo itatiwa sahihi na maafisa wawili kati ya wafuatao kama **kanuni zitakavyoelekeza**:

47.3.1. Rais wa Shirikisho
47.3.2. Makamu wa Rais
47.3.3. Mweka Hazina
47.3.4. Katibu Mkuu
47.3.5. Kamishina

Malipo yoyote ya fedha yataidhinishwa na Raisi wa shirikisho kwa kumshirikisha afisa mhasibu wa Shirikisho.

## IBARA YA 48: HESABU

48.1. Mwaka wa fedha wa shirikisho utakuwa tarehe 01 Januari hadi 31 Desemba kila mwaka.
48.2. Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na Wakaguzi wa Hesabu wa nje zitawasilishwa kwenye mkutano wa bodi ya Shirikisho kila mwaka.
48.3. Wakaguzi wa Hesabu watateuliwa na mkutano mkuu wa TBF.
48.4. Rais wa Shirikisho, Makamu wa Rais, Katibu mkuu na kamishina wa mipango na maendeleo wanaweza kuitisha na kuangalia utunzaji wa vitabu vya hesabu kutoka kwa mtunza hazina wakati wowote itakapohitajika kufanya hivyo.
48.5. Nakala ya Taarifa ya hesabu itapelekwa kwa Mwenyekiti Bodi ya wadhamini.
48.6. Mali za Shirikisho lazima zinakiliwe katika daftari la mali za TBF na kutunzwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu.

# SURA YA 9

# HATI MILIKI, NEMBO, BENDERA NA LUGHA

## IBARA YA 49: BENDERA

49.1. Shirikisho litakuwa na Bendera yake yenye rangi ya bluu bahari na nembo ya shirikisho katikati.
49.2. Bendera itapeperushwa na wajumbe wa bodi na kwenye ofisi za Shirikisho.
49.3. Bendera itapeperushwa kwenye mashindano yote yanayotambuliwa rasmi na shirikisho.

## IBARA YA 50: NEMBO

50.1. Kutakuwepo na nembo ya shirikisho.
50.2. Nembo ya Shirikisho ita ashiria vigezo vyote (i.e. rangi za nchi, aina ya mchezo, jina na alama nyingine zote zitakazo saidia kuutangaza na kuuza mchezo).

## IBARA YA 51: LUGHA

51.1. Lugha rasmi katika shughuli zote za Shirikisho ni Kiswahili na Kingereza. Lugha hizi pekee ndizo zitakazo tumika katika vikao na mawasiliano mengine.
51.2. Ikitokea kutokueleweka au kuchanganyika kwa baadhi ya vifungu vya katiba hii: Tafsiri ya lugha ya Kiswahili itafuatwa.

## IBARA YA 52: UAMUZI WA KUVUNJA SHIRIKISHO

52.1. Shirikisho litavunjwa kwa mujibu wa Sheria za Michezo nchini, chini ya usimamizi wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.
52.2. Mchakato wa kuvunjwa Shirikisho utaanzishwa kupitia uamuzi wa Mkutano Mkuu kwa kushirikisha Baraza la Wadhamini, Mlezi na BMT.

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## IBARA YA 53: KUPITISHA KATIBA

Katiba hii imepitishwa kwa matumizi kuanzia **11-Novemba-2020**.

Kwa tamko la pamoja la mkutano mkuu wa katiba uliofanyika tarehe **11 Novemba 2020**, katika ukumbi wa **Chuo cha Ufundi Don Bosco Dodoma** unafuta katiba ya awali ya Chama cha Mpira wa kikapu Tanzania. (TBF) iliyo anza kutumika tarehe **21-Oktoba-2001** na kufanyiwa maboresho tarehe **18-Juni-2024**.

**Katibu Mkuu**
Mwenze Kabinda
Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF)

**Rais**
Michael Kadebe
Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF)

OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
05 MAY 2025
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA